

فَقِيْهُ الْاِصْنَاءِ

FIQHI YA MAMBO YA SAUMU

Mtunzi:

Sheikh Haytham Bin Sarhan

Tarjama:

Abu Halima Arafat Bin Mahmoud

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

MAANA YA SAUMU:

Maana ya Saumu katika lugha ya kiarabu ni: kujizuia.

Na Kisheria ni: Kumuabudu Allaah kwa kujizuia kula, kunywa na baki ya vyenye kufunguza, tangu kuchomoza kwa alfajri ya kweli hadi kuzama kwa jua.

NGUZO ZA SAUMU:

Nguzo za saumu ni mbili:

1. Nia/Kunuwia.
2. Kujizuia na vyote vyenye kufunguza.

VIGAWANYO VYA NIA KATIKA SAUMU:

1. Nia ya saumu ya faradhi, ni lazima mtu anuwie tangu usiku kabla ya kuchomoza alfajri, na inatosheleza kunuwia (nia ya mwezi mzima) tangu kuandama kwa mwezi⁽¹⁾. Na Nia mahali pake ni moyoni wala haijathibiti kutamka, kwa hiyo kutamka Nia ni miongoni mwa bidaa.
2. Ama Nia ya saumu ya sunna inajuzu kunuwia katika wakati wowote wa mchana, muda wa kuwa hajakula kitu chochote (au kufanya jambo lenye kufunguza, kama vile tendo la ndoa n.k.) lakini ujira wa funga utazingatiwa pale atakaponuwia.

VIGAWANYO VYA SAUMU

Saumu ni aina mbili:

1. Saumu ya wajibu: kama vile Ramadhani, Kafara na Nadhiri.
2. Saumu ya sunna.

¹- Endapo aliacha kufunga kwa sababu ya maradhi au mwanamke alipata Hedhi, atanuwia tena kufunga masiku yaliyobaki ukiondoka udhuru huo.

MASHARTI YA YANAYOPASA KATIKA SAUMU YA RAMADHANI

1. Uislamu.
2. Akili timamu.
3. Baleghe (ama mtoto mwenye kupambanua-Mumayyiz- anatakiwa walii wake amuamrishe kufunga na kumsisitiza).
4. Awe ni mkazi (haipasi saumu kwa msafiri masafa ya kupunguza swala, na iliyo bora zaidi ni kufunga endapo hatopata tabu wala mashaka yoyote, kwa sababu ya kumuiga Mtume-Swala na Salamu zimshukie-, kuharakisha kujitoa katika dhima, na kudiriki fadhila za mwezi).
5. Afya, (ama mgonjwa si wajibu kwake kufunga na atakuja kulipa masiku hayo baada ya kupona).
6. Kuepukana na Hedhi na Nifasi (kwa mwanamke).

MARADHI/UGONJWA KATIKA SAUMU NI AINA MBILI

1. Mgonjwa ambaye haitarajiwi kwake kupona, atatoa fidia ya kulisha masikini mmoja kwa kila siku ambayo hakufunga, au atawakusanya (masikini sitini) na kuwalisha chakula kwa idadi ya siku ambazo hakufunga, pia ataingia katika hukumu hii mtu mzima sana ambaye atapata madhara endapo atafunga, na kiwango cha kulisha ni nusu ya pishi ambayo ni sawa na kilo moja na robo.
2. Mgonjwa ambaye hawezi kufunga lakini inatarajiwa kwake kupona, atafunga idadi ya masiku ambayo alifungua (alikula mchana), pia ataingia katika hukumu hii mwanamke mwenye Hedhi na Nifasi, kadhalika mwanamke mwenye mimba na mwenye kunyonyesha, na msafiri pia (wote hao ukimalizika udhuru wao watafunga siku zote ambazo walikula mchana), na lau mgonjwa alifariki kabla ya hajapona na hakuweza kufunga au mwanamke alifariki kabla kuondoka udhuru wake kadhalika msafiri wala hakuna chochote juu yake.

MAMBO YENYE KUFUNGUZA

1. Kula au kunywa katika mchana wa Ramadhani kwa makusudi, ama mwenye kusahau saumu yake ni sahihi.
2. Kufanya jimai (tendo la ndoa) mchana wa Ramadhani, kwa mtu ambaye ni wajibu kufunga, itamlazimu yeye kutoa kafara kubwa, ambayo ni kuacha mtumwa huru, akishindwa atafunga miezi miwili mfululizo, na asipoweza atalisha masikini sitini.
3. Kuteremsha (kutokwa na) manii kwa sababu ya kukumbatia, kubusu na mfano wake.
4. Kutumia kitu chenye kuchukua nafasi ya chakula na kunywa, kama vile sindano za vitamin c, ama sindano za kawaida hazifunguzi.
5. Kutoa damu kwa kufanya Hijama au kupiga chuku⁽²⁾, ama kutoa damu chache kwa ajili ya kupima malaria n.k jambo hili halifunguzi.
6. Kujitapisha.
7. Kutokwa na damu ya Hedhi au Nifasi.

MAMBO YA SUNNAH KWA MFUNGAJI

1. Kula daku.
2. Kuchelewesha kula daku (kuanzia theluthi ya mwisho ya usiku).
3. Kuharakisha kufuturu (baada tu ya kuzama kwa jua).
4. Kuanza kufuturu kwa tende ya Rutwab, na asipoipata basi kwa tende za kawaida, na iwe kwa idadi ya witri (moja, tatu, tano n.k), na asipopata afungue kwa tama/fumba la maji, na akiwa hakupata chochote basi atanuwia kufuturu kwa moyo wake.
5. Kuomba dua wakati wa kufuturu, na pia ukiwa umefunga.
6. Kukithirisha kutoa sadaka.
7. Kujitahidi kuswali swala za usiku.
8. Kusoma Qur'an kwa wingi.

²- Jambo hili wanachuoni wametafautiana, kuna wanaosema kwamba inafaa, kwa sababu hadithi ya kukataza kufanya Hijama kwa mfungaji imefutwa hukumu yake kwa hadithi nyingine yenye kuruhusu jambo hilo, na wengine wanaona kwamba atafungua endapo atachoka sana na kudhoofika. Ama damu inayomtoka mtu puani au kwenye jipu, vipele, kung'oa jino au kuchomwa na kitu cha ncha kali n.k, yote hayo hayabatilishi saumu.

9. Kufanya Umra.
10. Kauli yake: **[Mimi nimefunga]**, kumjibu yule aliyemtukana.
11. Kujitahidi kuutafuta usiku wa Laylatul Qadr.
12. Kukaa Itikafu katika kumi la mwisho la Ramadhani.

MAMBO YA MUBAHA (HALALI KUFANYA) KWA MFUNGAJI

1. Kumeza mate.
2. Kuonja chakula ikihitajika (lakini bila kumeza).
3. Kuoga mchana.
4. Kupiga mswaki.
5. Kujitia manukato (parfume).
6. Kuoga au kujimwagia maji baridi kichwani, kwa sababu ya kiu au joto kali.

MAMBO YA HARAMU KWA MFUNGAJI

1. Kumeza kohozi (lakini halifunguzi).
2. Kubusu, endapo haogopi kuharibu saumu yake kwa kutokwa na manii n.k.
3. Kusema uwongo, au kufanya jambo lolote la haramu.
4. Kufanya mambo ya ujinga na upuuzi.

SAUMU ZA SUNNAH

1. Kufunga siku sita katika mwezi wa Shawwaal, kwa yule aliyekamilisha kufunga Ramadhani, ataanza tu baada ya siku ya Eid.
2. Kufunga siku ya 'Arafa kwa mtu ambaye hakuhudhuria 'Arafa.
3. Kufunga siku ya 'Ashuraa (tarehe 9, 10 na 11 au 9 na 10 au 10 tu).
4. Kufunga siku ya jumatatu na alkhamis.
5. Kufunga siku tatu kila mwezi, na iliyo kufunga tarehe 13, 14 na 15.
6. Kufunga siku moja na kufungua siku moja (saumu ya Nabii Daud).
7. Kufunga mwezi wa Muharram.
8. Kufunga mwezi wa Sha'bani

SIKU AMBAZO NI KARAHYA KUFUNGA

1. Kufunga siku ya Ijumaa pekee.
2. Kufunga siku ya jumamosi pekee.
3. Kufunga siku ya jumapili pekee.

Lakini ikiwa mtu amefunga saumu maalumu, kama vile Kafara au Nadhiri, au imeafikiana na siku ya 'Arafa n.k. inajuzu wala hapana vibaya.

SIKU AMBAZO NI HARAMU KUFUNGA

1. Kufunga mwezi mzima wa Rajab au kuchagua baadhi ya siku kwa kuitakidi ubora au kuna fadhila zaidi kuliko siku nyingine, (ama yule mwenye kawaida ya kufunga sunnah hapana vibaya kufunga).
2. Kufunga siku ya shaka (nayo ni tarehe thelathini ya mwezi wa sha'bani, ikiwa kuna shaka, je mwezi ulionekana au haukuonekana?).
3. Kufunga siku za Eid mbili (Eid al Fitr na Eid al Adh-ha).
4. Kufunga siku za Tashriiq (siku tatu baada ya Eid al adh-ha, tarehe 11,12 na 13). isipokuwa kwa mtu ambaye amekosa mnyama wa kuchinja huko Makka (itafaa kwake kufunga katika siku za Tashriiq).
5. Kufunga milele.

Inapendekezwa kwa mwenye kulipa saumu afanye haraka baada tu ya siku ya Eid, wala haifai kuchelewesha mpaka kuingia Ramadhani nyingine, na lau alichelewesha kulipa mpaka ikaingia Ramadhani nyingine, hakuna juu yake zaidi ya kulipa siku hizo alizoacha.

ZAKATUL FITR

Inapasa Zakatul Fitr kwa kutoa pishi ya chakula kinachopendwa sana katika mji, atatoa yule ambaye limezama jua siku ya mwisho ya Ramadhani, hali ya kuwa yeye ni muislamu, (hata kama ni mtoto ambaye amezaliwa muda mchache kabla ya kuzama jua), na amiliki chakula cha mchana wa siku ya Eid na usiku wake, yeye pamoja na familia yake.

HEKIMA YA KUWEKWA ZAKATUL FITR

1. Kumtwaharisha mfungaji kutokana na maneno ya upuuzi aliyoongea akiwa amefunga.
2. Kuwatosheleza masikini na kutokuwa omba omba siku ya Eid.

WAKATI WA KUTOA KWAKE

1. Wakati unaojuzu, ni kabla ya siku ya Eid kwa siku moja au mbili. Inaruhusiwa kwa mtu kuipeleka Zakatul Fitr yake kwa siku moja au mbili kwa mtu ambaye anahusika na kuikusanya.
2. Wakati unaopendekezwa, baada ya swala ya alfajri na kabla ya kutoka Kwenda kuswali swala ya Eid.
3. Wakati wa haramu, baada ya kumaliza kuswali Eid, (isipokuwa kwa mtu mwenye dharura, kama kukosa wa kumpa n.k).

KIWANGO CHAKE

Kiwango cha kila mtu mmoja ni kutoa pishi moja ya chakula kinachopendwa sana katika mji wake, na wala haifai kutoa pesa.

Na kiwango cha pishi moja kwa vipimo vya kisasa ni kilo mbili na gramu arobaini.

SWALA YA EID

- **Hukumu yake:** Swala ya Eid ni faradhi ya lazima kwa kila mtu isipokuwa mwenye dharura.
- **Wakati wake:** Inaswaliwa baada ya kupanda kwa jua kiasi cha upinde (dakika 13-15) na mwisho wake ni kupinduka kwa jua.
- **Mahali pa kuswalia:** Sunnah ni kuswaliwa viwanjani nje ya mji, na inajuzu kuswali ndani ya msikiti (ikishindikana kuswali viwanjani).
- Sunna ni kula tende kwa idadi ya witri kabla ya kwenda kuswali Eid al Fitr, (ama swala ya Eid al Adh-ha sunna ni kula baada ya kurudi kuswali).
- Kuoga, kujitia manukato na kuvaa nguo nzuri.
- Kurudi na njia nyingine tafauti na ile uliyopita wakati wa kwenda.
- Hapana vibaya kupeana pongezi za Eid, kwa kusema: **(Taqabbala Allaahu minnaa waminkum)** n.k.
- Ni sunnah kusoma Takbira kuanzia usiku wa kuamkia Eid mpaka atakapokuja imamu kwa ajili ya swala, na kila baada ya kumaliza swala za faradhi, utasema **“Allaahu akbar, Allaahu akbar, Laa ilaaha Illa Allaah wallaahu akbar, Allaahu akbar walillaahil hamdu”**. Na katika Eid al Adh-ha zitaendelea Takbira mpaka siku ya tarehe 13 baada ya alasiri.
- Swala ya Eid ni rakaa mbili kabla ya khutba, katika rakaa ya kwanza atasoma Takbira sita ukitoa Takbira ya kuhirimia, na katika rakaa ya pili ni Takbira tano ukiacha Takbira aliyosoma wakati wa kunyanyuka, na utosoma Takbira hizi kabla ya kuanza kusoma (katika rakaa ya pili).

Abu Halima Arafat Bin Mahmoud.

25/Shab'ban/1445^H – 6/3/2024^M.

Pongwe Tanga.